HOTUBA YA MKUU WA SHULE BIBI HALIMA BARUGAHARE KAMOTE KWENYE SHEREHE ZA KUADHIMISHA MIAKA 17 YA SHULE NA MAHAFALI YA 15 YA KIDATO CHA 4, JUMATATU TAREHE 25 SEPTEMBA 2017, ENEO LA LUGURUNI, KATA YA KWEMBE, WILAYA YA UBUNGO, DAR ES SALAAM

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Azam Zungu, Mwenyekiti wa Bunge la Jamhuri ya Tanzania, mwakilishi wa Mh. Job Yustino Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Tanzania;

Mheshimiwa Mwenyekiti Mwanzilishiwa Joha Trust Professa Anna Tibaijuka, Mbunge Muleba Kusini

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Barbro Johansson, Bwana Salmon Odunga, wajumbe wa bodi na waanzilishi;

Afisa Taaluma wa Manispaa ya Ubungo Bibi Annert Nara na viongozi wa Serikali mliopo katika hafla hii;

Viongozi wa Mtaa wa Kwembe;

Mwenyekiti wa Umoja wa Wazazi na Walimu (PTA), Dr. John Kyaruzi na Kamati nzima ya PTA ya sasa na zilizotangulia;

Wakuu wa Shule, Walimu na Wanafunzi kutoka Shule za Sekondari jirani na zile za Mradi wa majaribio wa kuboresha elimu kwa mtoto wa kike;

Wahitimu wa Kidato cha IV, wanafunzi na wanajumuia wote wa Shule ya Barbro Johansson;

Wazazi na Wageni waalikwa;

Waandishi wa habari;

Mabibi na Mabwana.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi;

Napenda kutumia fursa hii kuungana na Mwenyekiti Mwanzilishi wa JOHA TRUST katika kuwakaribisha wageni wote ambao mmekuja kuungana nasi kusheherekea maadhimisho ya miaka 17 ya Shule na mahafali ya 15 ya kidato cha 4 kwa wanafunzi wetu 116 ambao watafanya mitihani yao ya taifa mwanzoni mwa mwezi Novemba 2017. Kwa niaba ya wana jumuia wa Shule ya Barbro nawakaribisha wote kwenye tukio hili muhimu la kihistoria.

Kwa namna ya pekee napenda kukushukuru wewe Mh. Azam Zungu kwa kukubali kushiriki pamoja nasi kufurahia na kuenzi vipaji mbalimbali vya wasichana wetu na pia kuwapongeza wahitimu na wafanyakazi wa Shule ya Barbro, pamoja na ratiba yako ngumu. Naamini ujio wako utahamasisha wasichana wetu na kuleta ushawishi katika kuhudumia wengine katika jamii zetu.

Natumia pia fursa hii kuwashukuru kwa dhati wale wote walioandaa shughuli hii hususan wafanyakazi na wanafunzi wa Shule ya Barbro. Namshukuru kila mmoja wenu kwa kutoa muda wake kuwa nasi leo.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Mabibi na Mabwana;

Katika kipindi cha miaka 17 tangu Shule kuanzishwa kuna mengi ya kusema kwani kama ni mtoto basi atakuwa amepitia hatua mbalimbali za ukuaji na sasa karibu atakuwa mtu mzima. Hata hivyo kutokana na muda tulio nao nitajikita katika kuelezea historia fupi, baadhi ya mafanikio, kuwatambua washirika wetu katika maendeleo, kuelezea changamoto na hatimaye kutoa neno la busara kwa wahitimu.
Kila mwaka sherehe kama hizi hufanyika tarehe 25 Septemba, siku aliyozaliwa Dk. Mama Barbro Johansson, ili kumuenzi mama huyu mmisionari, mwalimu mahiri, mwana harakati na mwana diplomasia. Mama Barbro atakumbukwa daima kwa mchango wake mkubwa katika kupigania elimu si tu kwa mtoto wa kike bali pia kwa mtoto wa kiume.

Shule ya Barbro ilianzishwa mwaka 2000 pale Ada estate, Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam, ikiwa na darasa anzilishi la kidato cha I lililokuwa na wasichana wahitaji 40 kutoka sehemu mbalimbali za Tanzania wote wakati huo wakisoma kwa ufadhili wa 100%.

Mwaka 2001, JOHA TRUST Tanzania na mfadhili mkuu kwa wakati huo SIDA kupitia ubalozi wa Sweden, Dar es Salaam, walifikia uamuzi wa pamoja wa kudahili pia wanafunzi ambao wazazi wao wanaweza kulipa ada. Uamuzi huu ulikuwa muhimu kwa ajili ya maendeleo endelevu ya Shule hasa baada ya kukoma kwa ufadhili kutoka kwa wahisani.

Mwaka 2002 Shule ilihamia hapa Luguruni baada ya kukamilisha ujenzi wa awamu ya kwanza katika eneo hili lenye ukubwa wa ekari 50 ambalo tulipewa na Serikali.

Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;

Katika miaka 17, Shule ya Barbro imekua, Kwa sasa Shule ina wanafunzi 643 kuanzia kidato cha I hadi cha VI, wafanyakazi 63 wakiwemo walimu 34 na wafanyakazi wengine 29. Masomo yanayofundishwa kwa kidato cha I hadi IV ni 14 yaani Hisabati, Kemia, Biolojia, Fizikia, Kompyuta, Kiswahili, Kiingereza, Fasihi za Kingereza, Kifaransa, Jiografia, Historia, Uraia, Biashara na Utunzaji wa Vitabu vya Fedha, Elimu ya dini ya kiislamu na Masomo ya Biblia. Tahasusi kwa wanafunzi wa vidato vya V na VI zipo 9 yaani PCM, PCB, CBG, EGM, ECA, HKL, HGL, HGE na HGK hivyo kuwapa wanafunzi wigo mpana wa uchaguzi wa masomo na tahsusi. Mwaka huu tutakuwa na mpango wa mafunzo ya awali kabla ya kuingia kidato cha kwanza yaani Pre- Form one kuanzia tarehe 7 Oktoba 2017. Fomu za maombi zinapatikana kwenye ofisi ya utawala au tovuti yetu www.johatrust.ac.tz.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi;

Tunayo pia shule dada huko Bukoba iitwayo Shule ya Sekondari ya Alexander Kajumulo ambayo ina wanafunzi 181 kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita. Hadi sasa shule ya Barbro hapa Luguruni imetoa wahitimu 1030 wa kidato cha nne na 934 wa kidato cha sita. Ukiongeza na hawa wahitimu 116 wa darasa la kidato cha nne tunapata jumla ya wahitimu wote kutoka shule hii kuwa 2080. Kati ya wahitimu waliotangulia, 99.9 walifaulu masomo yao katika viwango vya kuwawezesha kuendelea katika ngazi nyingine za elimu.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, mabibi na mabwana;

Shule ya Barbro haikuachwa nyuma katika mashindano mbalimbali yakiwemo kuandika insha, chemsha bongo na mambo yahusuyo taaluma. Mara nyingi tumeibuka washindi kama ambavyo mmejionea

kwenye vyeti mbalimbali vya ushindi ambavyo tumevionesha kwenye ubao wa matangazo nje ya jengo la utawala. Mwaka huu wanafunzi wetu walionesha umahiri mkubwa kwenye mashindano ya mdahalo yaliyofanyika Zanzibar ambapo washiriki walikuwa wanafunzi kutoka Shule za Sekondari za Barbro Johansso, Feza, Al Muntazir na Mtakuja na vyuo vikuu vya Tanzania, Nigeria, Zimbabwe, Kenya, Afrika kusini na Cameroon. Katika mashindano haya timu ya Shule ya Barbro ya wanafunzi Joan Mshona na Nasra Mohamed wa kidato cha 6 iliibuka mshindi wa pili. Vilevile mwanafunzi wetu Thecla Ngwilimi Kidato cha 6 aliibuka kuwa mshindi bora wa kwanza katika mdahalo (yaani Best overall debator) na Nasra Mohammed Kidato cha 6 mshindi bora wa pili katika kuongea kwenye kadamnasi (yaani second best Public Speaker).

Vilevile mwanafunzi wetu Brenda Ngatala wa kidato cha sita alichaguliwa kushiriki katika kambi ya wasichana ya Sayansi huko nchini Malawi kuanzia tarehe 29 Julai hadi 16 Agosti mwaka huu 2017 ambapo nchi kadhaa zikiwemo Marekani, Liberia, Malawi, Uganda, Zambia, Rwanda na Tanzania zilishiriki. Kambi hiyo iliendeshwa na Ubalozi wa Marekani ikishirikiana na taasisi nyingine kama Google, NASA, Intel na US Department of State ambapo washiriki walijifunza mambo mbalimbali kuhusu technologia. Huko nako pia, Brenda na timu yake waliibuka kidedea na kuwa timu bora katika mradi walioubuni wa kutumia teknologia katika kutengeneza maabara shuleni.

Halikadhalika Shule imewezesha kukuza vipaji mbalimbali katika uongozi, Sanaa za ubunifu, maigizo, uimbaji, ngoma, muziki wa kisasa na michezo mbalimbali na kujenga mahusiano mema na shule nyingine kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi;

Mpango wa kubadilishana walimu na wanafunzi na shule rafiki nchini Sweden umeendelea kutekelezwa kwa takriban miaka 13 sasa. Wanafunzi wawili (2) waliomaliza kidato cha nne 2016; Agnes Komungoma na Swalha Seleman walikwenda Sweden katika program hiyo kwa mwezi mmoja mwanzoni mwa mwaka huu. Halikadhalika wanafunzi 4 kutokea Sweden walikuja Barbro kwa mwezi mmoja na nusu kuanzia Julai hadi August mwaka huu katika mpango huo. Tunatarajia wanafunzi wetu 10 na mwalimu mmoja watakuwa na ziara nchini Sweden kwa muda wa wiki mbili mwishoni mwa mwezi Novemba chini ya mpango huo. Mpango huu umesaidia katika kupata uelewa na kujenga uhusiano wa kiutamaduni kimataifa, kutoa fursa za kubadilishana fikra, uzoefu, elimu na ujuzi katika mambo ya kitaaluma na kijamii baina yetu na shule rafiki za Sweden.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi;

Shule inaendelea kutekeleza mpango wa kuwafikia wasichana wanaotoka kwenye familia zenye uhitaji. Kwa kupitia mpango huu wasichana wanaotokea kwenye familia hizo wengine mbali mikoani, wamefikiwa na wamenufaika. Kwa sasa 8% ya wanafunzi wetu wananufaika na ufadhili wa ada. Tunawashukuru washirika wetu wa maendeleo JOHAFONDEN chini ya Mwenyekiti Mama Gun Britt Andersson na Mama mlezi Lizbeth Palme kwa kuendelea kuwezesha mpango huu kifedha. Mwaka huu pekee JOHA FONDEN imetoa SEK 750,000 sawa na wastani wa shilingi 186 milioni kwa ajili ya ufadhili wa ada ya wanafunzi wahitaji. JOHAFONDEN pia wameisaidia shule kukua kitaaluma kwa kutoa vifaa mbalimbali vya masomo na kufadhili mafunzo, semina na warsha kwa walimu wetu.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, mabibi na mabwana;

Shule ya Barbro imeendelea kutekeleza mradi unaofadhiliwa na Forum Syd wa kueneza Mambo mema ya Shule ya Barbro katika uboreshaji wa Elimu kwenye Shule nyingine za mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Mradi huu wa majaribio, ambao ulianza Agosti 2015 na kutarajiwa kumalizika Mei 2018, unahusisha shule tano zikiwemo Shule za Sekondari za Kwembe na Bethsaida (wilaya ya Ubungo), Majani ya Chai (Ilala), Chang'ombe (Temeke) na Shule ya Sekondari ya Wasichana Kibaha ambapo Shule ya Barbro inashirikisha shule hizo kufahamu na kutumia mbinu mbalimbali tulizotumia katika kuboresha elimu hususan kwa mtoto wa kike, kwa lengo la kuboresha elimu katika shule shirikishi na hatimaye kusambaza mbinu hizi kwa shule nyingi zaidi. Nafurahi shule hizo zimewakilishwa katika hafla hii. Tayari matokeo ya kutia moyo yameanza kuonekana katika shule shiriki hususan kwenye nidhamu chanya, masomo ya ziada, klabu za wanafunzi, ushauri nasaha na ushirikishwaji wa wazazi kupitia PTA, zikiwa ndizo nguzo zilizotiliwa mkazo na mradi. Tunawashukuru tena rafiki zetu wa Joha Trust Sweden kwa kutafuta fedha kutoka Forum Syd kwa ajili ya mradi huu.

Mabibi na mabwana;
Uhusiano mwema kati ya walimu na wazazi wa Shule ya Barbro katika malezi ya wanafunzi umeendelea kudumishwa. Shule iliandaa na kufanya semina za malezi ya watoto na kuwasaidia wanafunzi katika uchaguzi wa masomo, ili kuwaandaa kwa kazi za baadae, kwa wazazi wa kidato cha kwanza tarehe 11 Februari 2017. Nao wazazi wa kidato cha tano walihudhuria semina kama hiyo tarehe 5 Agosti 2017. Tunaamini ya kuwa semina hizi zimekuwa za manufaa kwetu sote.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi;

Tunapoongelea juu ya maendeleo tukumbuke kuwa kuna watu ambao wametoa mchango mkubwa kuleta maendeleo hayo. Mradi huu wa shule usingeweza kuwepo bila ya kuwa na waanzilishi mahiri. Naomba kutumia fursa hii kumshukuru Hayati balozi Wilson Tibaijuka ambaye alikuwa Mwenyekiti wa kwanza wa JOHA TRUST (Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi), Mwenyekiti Mwanzilishi, Mheshimiwa Professa Anna Tibaijuka, Wajumbe wa Bodi na washauri chini ya Mwenyekiti Bwana Salmon Odunga na Mlezi Balozi Paul Rupia, ambao wametoa muda wao mwingi, akili na nguvu, ili kuhakikisha kwamba mradi huu unafanikiwa.

Napenda kutumia fursa hii pia kuwashukuru wale wote ambao michango yao ya mawazo hali na mali imetufikisha hapa tulipo.

Kwanza kabisa ni Serikali ya Tanzania ambayo imetupatia ekari 50 za ardhi hii ya hapa shuleni ambayo tunajivunia, miundombinu mbalimbali ikiwemo barabara, maji na umeme, usajili wa shule, ukaguzi, mitihani ya taifa na ushirikishwaji katika kutoa elimu.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi;

Shule hii isingefika hapa ilipo kama si msaada mkubwa uliotolewa na Serikali ya Sweden kupitia Ubalozi wa Sweden hapa Dar es salaam kwa miaka 12 kuanzia 2000 hadi 2012. Msaada huu ulitumika kwa ujenzi na kufadhili wasichana waliotokea kwenye mazingira magumu. Niwahakikishie ndugu zetu wa Sweden kuwa mti mliopanda utaendelea kuzaa matunda yatakayolisha wengi kwa muda mrefu ujao.

Mabibi na Mabwana;

Nitakuwa mchoyo wa fadhila iwapo sitawashukuru wazazi wa Shule hii chini ya Mwenyekiti Dk John Kyaruzi. Wazazi wamekuwa wadau wetu wakuu, tukishirikiana bega kwa bega katika kuleta maendeleo ya shule hususan katika misaada kwa wanafunzi wetu wahitaji, kuchangia maendeleo katika masomo na mambo ya kijamii. Sasa hivi wazazi wako kwenye harambee kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kisasa la Maktaba na Tehama, mbali na ushirikiano mkubwa wanaotupatia katika kutekeleza mradi wa kusambaza mambo mema ya Barbro ambao nimeuelezea awali.

Ki uhalisia siyo rahisi kumshukuru kila aliyejitoa kusaidia maendeleo ya shule hii kwa kuwa orodha ni ndefu lakini niseme tu kwamba asanteni sana wote kwa kutuunga mkono.

Mheshimiwa mgeni Rasmi;

Pamoja na maendeleo tuliyofikia, Shule inakabiliwa pia na changamoto:

Kutokana na ugumu wa upatikanaji wa fedha na ufinyu wa bajeti ujenzi wa miundo mbinu kama ilivyo katika Mpango Mkuu wa Shule unaenda polepole. Majengo kama Madarasa, Ukumbi wa kukusanyikia, Maktaba, Nyumba za Wafanyakazi, Miundombinu ya Michezo, Barabara za Ndani, n.k hayajakamilika.

Wageni Waalikwa;

Utafutaji wa fedha za kutosha kwa ajili ya kufadhili wasichana wanaotoka kwenye familia zenye uhitaji umekuwa siyo rahisi. Hilo limeleta moja kwa moja athari katika kudahili na kusajili wanafunzi wahitaji hapa shuleni. Tayari JOHA TRUST imelazimika kukubali hali halisi na kupunguza idadi ya wasichana wanaofadhiliwa kutoka 100% mwaka 2000 tulipoanza na polepole idadi hii imepunguzwa hadi kufikia 8% mwaka huu 2017.

Changamoto kubwa zaidi ni kudumisha viwango vya ubora kwa bajeti finyu iliyopo.

Mheshimiwa Mgeni wetu Rasmi mabibi na mabwana;

Katika majukumu uliyo nayo leo ni pamoja na kutunuku makundi mbalimbali. Tunao walimu waliofanya vizuri zaidi ya wengine katika mitihani ya taifa na wapo waliodumu kazini kwa muda mrefu wa miaka 10 na 15. Pia tunaye mfanyakazi bora wa mwaka 2017. Hawa wote tutaomba uwape tuzo kama ishara ya shukrani kwa kufanya vizuri zaidi ya wengine na kutambua mchango wao kwa shule. Halikadhalika wapo wanafunzi ambao utawapa tuzo kwa kufanya vizuri kwenye masomo, uongozi, nidhamu, michezo, n.k. Hatimaye tutakuomba uwatunuku vyeti wahitimu wetu wa kidato cha nne.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi;

Kwa ridhaa yako naomba sasa niwageukie wanafunzi wahitimu. Tunao wahitimu wa kidato cha nne 116 na wote wamefanya vizuri katika masomo yao. Kama usemi wa Kiswahili usemavyo “Mcheza kwao hutunzwa” hivyo punde utawapongeza kwa veti vya kuhitimu. Wasichana hawa wana utashi na matarajio makubwa. Shule imewaandaa kujiwekea malengo ya juu katika maisha na hakuna shaka wote watafanikiwa katika malengo waliyojiwekea. Wengi wao wamekuwa nasi kwa miaka mine sasa lakini bila kujali muda tuliokuwa nao shuleni tumejitahidi kuwapa mafunzo stahili, elimu na ujuzi.

Enyi wanangu mnaohitimu;
Sherehe za mahafali kama ya leo ni siku maalum ambapo mnafikia kilele cha miaka ya kazi ngumu, kupata uhalisia wa malengo mliojiwekea na kuthibitisha mafanikio mliyofikia. Kwa hiyo ni sahihi tukumbuke barabara tuliyosafiri pamoja kwa miaka hii michache iliyopita. Imekuwa ni safari ambayo pengine ilianza kwa hatua za majaribio lakini hatimaye imetufikisha kwenye kilele. Katika safari hii tumekutana na majaribu na taabu lakini tulijikaza kiume na hivyo kujenga umahiri. Vilevile tumekuwa na matukio mbalimbali mazuri na ya kipekee ambayo yatakumbukwa kwa miaka mingi ijayo.

Wakati tunaangalia miaka kadhaa nyuma ni dhahiri kulikuwa na mwanzo, tunashukuru kumekuwa na maendeleo na hakika tumefanikiwa. Leo napenda niwausie mambo kadhaa:

1. Msiache kujifunza, tafadhali chukueni sehemu ya shule huko mwendako na mtagundua kuwa si tu kwamba mmepata elimu na ujuzi bali pia mmebeba historia, maadili, mila na desturi za taasisi yakiwemo upendo, huruma, wema, busara, ubunifu, uvumilivu, heshima, na uthubutu na myatumie hayo katika kuleta mabadiliko chanya po pote mwendako.
2. Waheshimuni watu wote nanyi pia mtaheshimiwa. Zaidi sana waheshimuni wazazi na walezi wenu ambao wamejitolea sana maishani kwa ajili yenu, msije mkang'ata mkono unaowalisha.
3. Siku zote muwe wakweli wa nafsi zenu. Katu msijaribu kuwa ambavyo sivyo mlivyo kwani kufanya hivyo mtakuwa mmejiandalia wenyewe kukosa matumaini na furaha.
4. Asilani hata mmoja wenu asifikiri ya kwamba yeye ni mtu mdogo sana au asiye na uwezo wa kuleta mabadiliko. Hakuna kosa kubwa kama mtu kutofanya cho chote wakati angefanya japo kidogo katika kuchangia mabadiliko.
5. Kuwa na ujasiri wa kukutana na watu tofauti na kujaribu mambo mema ambayo hujawahi kuyafanya kabla.
6. Kuweni na ndoto kubwa katika maisha. Sisi tunaamini tumewafunza kuwa dhabiti na tumewaandaa kuwa jasiri na wavumilivu ili kuwawezesha kufanikiwa na kushinda vikwazo vyote mtakavyokumbana navyo maishani.
7. Dumisheni urafiki mlioujenga mkiwa hapa shuleni lakini msing'ang'anie tu rafiki ambao mnafanana lakini wafikieni na kuwasikiliza wale wanaotoka kwenye mazingira na mitazamo tofauti, na cha muhimu zaidi jitoleeni sehemu ya muda wenu kwa ajili ya wengine.
8. Msiogope kujaribu na kushindwa. Ni rahisi wakati mwingine kuhisi umeshindwa lakini nyakati kama hizi zione kama changamoto, mawazo chanya huleta mafanikio chanya. Jifunze kutokana na makosa na ustahmili kwani watu ambao hawana furaha katika dunia hii inawezekana hawajawahi kushindwa cho chote.
9. Furaha iwe ndio chaguo lako. Fikira zako ni zako mwenyewe na zitatoa taswira ya mtazamo wako wa ulimwengu huu.
10. Kumbuka kuwa watu wengi wana imani nanyi na wamewekeza sana kuwasaidia kufanikiwa. Sasa ni zamu yenu kuonesha mafanikio katika mitihani yenu ijayo kwani elimu hii mliyopata ni mwanzo tu wa safari nyingine ya elimu ya juu ya sekondari na hatimaye vyuo vikuu.

Kwa hiyo wanangu, kwa niaba ya wana jumuia ya Barbro nawatakia kheri na Baraka nyingi katika mitihani yenu ya taifa na yote mnayostahili katika miaka ijayo.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Mabibi na Mabwana;
Napenda kuhitimisha kwa kusisitiza kuwa tunahitaji nguvu za pamoja kwa maendeleo endelevu ya Shule ya Barbro na taifa kwa ujumla. Karibuni tuifurahie pamoja siku hii ya muhimu na ya kihistoria.

Asanteni kwa kwa kunisikiliza.